**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**
**WILAYA YA UKEREWE**

## MUONGOZO KIDATO CHA KWANZA KISWAHILI.

1 ALAMA 10@01

| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) | (viii) | (ix) | (X) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | C | C | B | D | C | A | B | C | B |

2 ALAMA 05 @01

| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|
| B | G | D | E | C |

3. (a) Umuhimu wa kamusi

- Kueleza maana ya neno
- Kueleza aina ya neno. **( Alama 5 @ 01)**
- Kueleza Umoja na wingi wa neno
- Kutoa mifano ua utumizi wa neno
- Kueleza maneno yenye maana sawa / tofauti

(b) Hadhi.ya lugha ya kiswahili

i)Hutumika katika shughuli rasmi za kimataifa
ii)Imefanikiwa kwa kiwango kikubwa kuleta umoja katika bara la Afrika
iii)Kishwahili.kinatumika kama.lugha rasmi katika jumuiya ya maendeleo kusini mwa Afrika SADC na jumuiya ya Afrika mashariki
iv)Kiswahili kimetoa fursa za ajira kimataifa **( Alama 5 @ 01)**
v)Kiswahili ndio lugha pekee inayotumika katika umoja wa Afrika sanjari na lugha nyinginezo

**4.** (a)Mwanafunzi aandike sentensi kwa.usahihi
i)Nipatie viatu vyangu tafadhali
ii)Baba amenunua mbuzi mnyama wa kufugwa
AU Baba amenunua kibao cha kukuna nazi

iii)Rehema amekwenda Iringa
iv)Tulipomaliza kula,tulilala
v)Nimekuelewa vizuri (**ALAMA 5 @ 1 )**

(b) Lugha - ni sauti za nasibu zenye kuleta maana ambazo zimekubaliwa na wanajamii kutumika kwa mawasiliano miongoni mwao. **Alama 1**

Mfumo wa lugha

i) Sauti ni sehemu ndogo kabisa ya neno isiyoweza kugawanywa Zaidi.

Mfano: b, a, t, a, (n.k)

ii) Silabi ni sehemu ya neno inayoundwa na sauti moja au Zaidi.

Mfano: b+a = ba, m+a =ma, n+y+a=nya (n.k)

iii) Maneno ni silabi moja au muunganiko wa silabi kuanzia mbili na Zaidi.

Mfano: ha+yu+po= hayupo

iv) Sentensi ni neno kuanzia moja na kuendelea yanayotoa ujumbe kamili.

Mfano: Njoo + myumbani = Njoo nyumani **Alama 4 @ 1**

5. i. **Lo! Mwanafunzi nadhifu amefaulu mtihani**

Lo! - Kihisishi

Mwanafunzi - Nomino

Nadhifu - Kivumishi

Amefaulu - Kitenzi

Mtihani - Nomino

ii. **Kokoto zile zimekusanywa na wanakijiji**

Kokoto - Nomino

Zile - Kivumishi kioneshi

Zimekusanywa - Kitenzi

Na - Kihusishi

Wanakijiji - Nomino

iii. **Yule amekwenda shuleni kwa miguu**

Yule - Kiwakilishi kioneshi

Amekwenda - Kitenzi

Shuleni - Kielezi

Kwa - Kihusishi

Miguu - Nomino

iv. **Mimi ninapenda kujifunza Kiswahili**

Mimi - Kiwakilishi nafsi

Ninapenda - Kitenzi

Kujifunza - Kitenzi

Kiswahili - Nomino

v. **Kijana huyu ni mtukutu sana**

Kijana - Nomino

Huyu - Kivumishi kioneshi

Ni - Kitenzi (kiunganishi)

Mtukutu - Kivumishi

Sana - Kielez

**Alama 10 @=2**

6 . (a)Mambo yakuzingatia katika kusoma kwa uafasha

i)matamshi sahihi ya maneno
ii)kuzingatia alama za uandishi
iii)kuzingatia mtiririko wa aya (ALAMA 5@1 )
iv)kasi stahiki
v)utamkaji sahihi wa silabi zenye mkazo na kiimbo katika maneno ili kupata maneno sahihi

(b) Umuhimu wa ufahau(ALAMA 5@1)

i) Huweza kukuza uelewa.wa mambo mbalimbali
ii) Husaidia kukuza uwezo wa kujenga hoja
iii) Husaidia katika uwezo wa kuchambua mambo
iv) Huchochea uwezo wa kujifunza mambo mbalimbali
v) husaidia uwezo wa kujieleza kwa ufupi na kwa ufasaha

**7. Kamusi**

(a) **Maana:**

- Kamusi ni kitabu kinachotoa maana, tafsiri, na matumizi ya maneno. **Alama 1**

(b) **Aina tatu:**

1. Kamusi ya Kiswahili-Kiswahili
2. Kamusi ya Kiswahili-Kiingereza
3. Kamusi ya istilahi za sayansi **Alama 1.5**

(c) **Jinsi ya kutumia kamusi:**

- Tafuta neno unalotaka kuelewa
- Soma maana yake na mfano
- Elewa matumizi yake katika sentensi **Alama 1.5**

**8. Muktadha wa mawasiliano**

**(a) Maana:**

 Muktadha ni mazingira au hali ya mawasiliano inayowezesha ujumbe kueleweka vizuri. . **Alama 1**

**(b) Mifano mitatu:**

a. Chumba cha darasa
b. Shule au ofisi
c. Shughuli za kijamii (mikutano, mikutano ya kijamii) **Alama 1.5**

**(c) Kanuni tatu za mawasiliano bora:**

a. Kuwa mkweli na sahihi
b. Kuheshimu msikilizaji
c. Kutumia lugha inayofaa muktadha **Alama 1.5**

9. **Mazungumzo vs Maandishi** (a)

**Tofauti:**

- Lugha ya mazungumzo hutumika mdomoni, mara nyingi isiyo rasmi.
- Lugha ya maandishi hutumika kuandika, mara nyingi ina kanuni na mpangilio maalumu. **Alama 4**

(b) **Mifano:**

- Mazungumzo: “Habari gani?”; “Unaendeleaje?”
- Maandishi: “Nimefurahi kukuona leo.”; “Tafadhali andika ripoti hii kwa

usahihi.” **Alama 4**

(c) **Faida za kuimudu lugha ya mazungumzo:**

1. Kuongeza uelewa kati ya watu
2. Kujenga uhusiano bora wa kijamii
3. Kuepuka migongano na misigano   Alama 3

ALAMA 10@02

10 Barua izingatie mambo yafuatayo;

(i) Anuani ya mwandishi 02

(ii) Tarehe 01

(iii) Utangulizi 02

(iv) Kiini 04

(v) Mwisho wa barua02

(vi) Jina la mwandishi ( 02)

(vii) Saini 02)